1. SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI – MKOA WA NJOMBE

1.1 Idadi ya watumishi

Halmashauri	Sekta	Waliopo	Upungufu	Jumla
Ludewa	Mifugo	24	51	7
	Uvuvi	3	15	1
Makete	Mifugo	18	59	7
	Uvuvi	0	4	
Wanging'ombe	Mifugo	27	81	10
	Uvuvi	1	3	
Njombe DC	Mifugo	14	39	5
	Uvuvi	0	3	
Mji Njombe	Mifugo	21	29	5
	Uvuvi	2	3	
Mji Makambako	Mifugo	19	49	6
	Uvuvi	0	3	
Njombe RS	Mifugo	2	0	
	Uvuvi	0	1	
Jumla kuu	**Mifugo**	**125**	**308**	**43**
	Uvuvi	**6**	**32**	3

Chanzo: Halmashauri -2023

1.2 Aina ya mifugo na idadi

Hadi kufikia Juni, 2023 Mkoa unakadiriwa kuwa na Ng'ombe wa asili **194,473** na wa maziwa **16,335,** Mbuzi wa asili **95,126,** na wa maziwa **6,225,** Kondoo **19,354,** Nguruwe **99,531,** Kuku wa kisasa **736,399,** na asili **1,131,596,** Mbwa **24,772,** Paka **13,395,** Punda **9,967,** Farasi **21,** Sungura **28,901,** Simbilisi **112,709**, Njiwa **4,662,** Kwale **89,** Bata **11,038,** na kanga **2,279.** Ufafanuzi zaidi umeoneshwa katika Jedwali hapa chini**.**

Jedwali.Na: 01 Idadi ya Mifugo Mkoa wa Njombe

Halmashauri	Ng'ombe		Mbuzi		Kondoo	Nguruwe	Kuku		Mbwa	Paka	Punda
	Asili	Kisasa	Asili	Kisasa			Asili	Kisasa			
Makambako	21,410	2,403	6,725	36	1,358	4,852	91750	201,522	3,811	669	75
Wanging'ombe	59071	3,945	23,001	156	2,951	24,607	289,761	48,407	2,902	1,232	680
Mji Njombe	20,626	4,368	13,142	41	4,026	18,849	51,889	288,261	5,205	6,935	2734
Ludewa DC	41763	737	2224	0	351	23,571	401,786	49,836	4,374	2,693	2226
Njombe DC	32,422	3,633	24567	2996	1,435	9,693	232,951	98,583	3,180	1,809	144
Makete DC	19181	1,249	25467	2996	9233	17,959	63,459	49,790	5,300	14,43	4108

Jumla	**194,473**	**16,335**	**95,126**	**6,225**	**19,354**	**99,531**	**1,131,596**	**736,399**	**24,772**	**13,395**	**9,967**
Jumla kuu	**210,808**		**101,351**		**19,354**	**99,531**	**1,867,995**		**24,772**	**13,395**	**9,967**

Miundombinu na Malisho ya mifugo

Mkoa wa Njombe una jumla ya majosho **106**, minada **5,** machinjio (slaughter haouse) **6,** vituo vya kutolea huduma za mifugo (veterinanry center) **60**, mabirika ya kunyweshea mifugo **69** na vituo vya kukusanyia maziwa **19.** Aidha, Mkoa una jumla ya hekta **280,533** zinazofaa kwa malisho na kati ya hizo Hekta **9,809** zimepandwa malisho bora aina ya *Rhodes na Elephant grass.*

1.3 Uzalishaji wa mazao ya mifugo

Katika Mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya kilo **7,290,473** za nyama zenye thamani ya shilingi **55,798,916,000,** mayai **82,909,900** yenye thamani ya shilingi **40,454,950,000,** maziwa lita **16,676,240** zenye thamani ya Shilingi **15,492,826,000** na ngozi **49,869** zenye thamani ya shilingi **84,109,000** zilizalishwa katika Mkoa wa Njombe.

1.4 Sekta ya Uvuvi katika Mkoa

Katika kuendeleza na kusimamia shughuli za ufugaji wa samaki katika mabwawa, Mkoa una jumla ya mabwawa ya Samaki **1,074,** vizimba (fish cages) **2** katika Halmashauri ya Ludewa. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya kilo **73,065** za Samaki wenye thamani ya shilingi **657,585,000.00** zilivunwa na kuuzwa.

2 SEKTA YA MISITU

2.1 Utangulizi

Hadi Oktoba, 2023 Mkoa una takribani hekta **401,400** za miti ya kupandwa na hadi hekta **263,320.83** na jumla ya hekta **664,720.83** zenye eneo la misitu kwa mkoa mzima sawa na asilimia **31.39** ya ardhi yote ya Mkoa.

Umiliki wa misitu kwa Mkoa huu, umegawanyika katika katika makundi tofauti kulingana na aina ya msitu. Misitu ya kupandwa inamilikiwa na watu binafsi (kwa kiasi kikubwa), taasisi, vikundi na kampuni kama TANWAT yenye mashamba makubwa.

Misitu ya asili ni ile ya Hifadhi Taifa inayomilikiwa na Wakala wa huduma za Misitu (TFS – Tanzania Forest Service Agency), Halmashauri za Wilaya, Vijiji na watu binafsi pamoja na misitu iliyopo katika Safu za Milima ya Livingstone na Kipengere.

2.2 Hali ya Upandaji Miti

Mkoa wa Njombe ni miongoni mwa mikoa inayoongoza hapa nchini kwa kupanda miti kwa lengo la kuongeza kipato cha kaya, Wilaya, Mkoa na Taifa kwa ujumla. Wananchi wa Mkoa huu wamekuwa na mwitikio chanya katika masuala yote ya upandaji miti ikiwemo ya Mbao, matunda, nishati (kuni, mkaa), mapambo na kuhifadhi mazingira ikiwemo vyanzo vya maji.

Mkoa umekuwa ukivuka lengo la Kitaifa la kila Halmashauri kupanda miti isiyopungua 1,500,000 kwa mwaka ambapo kwa msimu wa upandaji miti wa mwaka 2022/2023 Mkoa ulipanda jumla ya miti 34,060 552 kupitia Halmashauri zote sita.

2.3 Mkoa wa Njombe mshindi wa banda bora kundi la mikoa kwenye maonesho ya utalii ya karibu kusini, 2023

Mkoa na Halmasahuri zake 6 ulishiriki kwenye Maonesho ya Utalii yajulikanayo kama Karibu Kusini yaliyofanyika Mkoani Iringa kuanzia atrehe 23 hadi 28 Septemba, 2023.

Maonesho hayo yalizinduliwa tarehe 23 Septemba, 2023 na Mgeni rasmi Mh. Angela Kairuki (Mb) Waziri wa Maliasili na Utalii. Mh Waziri alitumia fursa hiyo kuelezea furs za utalii zilizopo Mikoa ya Kusini na Mikakati ya kuendeleza fursa hizo ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu mbalimbali kwenye vivutio vya Utalii. Pia aliaezea mipango mbalimbali iliyopo ya kuendeleza Kituo cha Utalii kwa Mikoa ya Kusini katika eneo la Kihesa Kilolo Manispaa ya Iringa.

Maonesho hayo yalifungwa na Mgeni Rasmi Mh. Exaud Kigahe (Mb) Naibu Waziri wa Viwanda na Uwekezaji tarehe 28/9/2023 kwa kutoa hotuba na maelekezo kwa mikoa ya kusini na kugawa zawadi za ushindi kwa makundi mbalimbali ambapo kwa Kundi la Mikoa, Mkowa Njombe umeshika nafasi ya Kwanza kuwa na Banda Bora,2023.

3 SEKTA YA UFUGAJI NYUKI

3.1 Utangulizi

Mwitiko wa wananchi katika kutekeleza shughuli za ufugaji wa nyuki ni mkubwa. Mkoa una jumla ya mizinga 25,796 ya kienyeji na 19,835 ya kisasa, ambapo kwa mwaka 2022/2023 jumla ya kilo 224,171.2 za asali na kilo 8,594.5 za nta zilizalishwa.

Uzalishaji huu unatokana na fursa nyingi za kuwekeza katika shughuli za ufugaji nyuki zikiwemo:-

1. Uwepo wa maeneo makubwa yaliyo na misitu ya asili na kupandwa inayoruhusu shughuli za ufugaji nyuki
2. Uwepo wa mashamba ya mazao mbalimbali ya kilimo yanayoruhusu shughuli za ufugaji nyuki.
3. Uwepo wa hali ya hewa inayoruhusu shughuli za ufugaji nyuki.
4. Uwepo wa miundombinu (barabara ambazo zinapitika misimu yote kutoka wilayani hadi mkoani)
5. Uwepo wa nishati ya umeme katika kila Makao Makuu ya Wilaya.
6. Uwepo wa wataalamu ngazi ya Wilaya na Mkoa
7. Uwepo wa sera, sheria na kanuni zinazoruhusu shughuli za ufugaji nyuki katika Mkoa.
8. Uwepo wa Wataalamu wa kutengeneza zana za kuendeshea shughuli za ufugaji nyuki kama vile mizinga na mavazi ya kujikinga.
9. Uwepo wa makundi mengi ya nyuki sehemu mbalimbali katika Mkoa.

Jedwali Na: 2 Uzalishaji wa Asali Mkoa wa Njombe kwa Mwaka 2022/2023

Halmashauri	Idadi ya Mizinga		Idadi ya Vikundi vya Ufugaji Nyuki	Uzalishaji wa zao la Asali na Nta 2022/23	
	Kienyeji	Kisasa		Asali (Kg)	Nta(Kg)
Njombe DC	3,858	5,482	35	54,151	1,615
Njombe TC	5,852	1,729	21	8,670.2	528.5
Ludewa DC	6,100	6,457	10	83,748	1,150
Makete DC	5,449	847	25	65,988	4,499
Makambako TC	15	57	2	272	63
Wanging'ombe DC	4,522	5,263	38	11,342	739
JUMLA	25,796	19,835	131	224,171.2	8,594.5

Chanzo: Halmashauri za Mkoa wa Njombe, 2023

3.2 Changamoto zilizopo katika shughuli za ufugaji wa nyuki

1. Ukosefu wa mitaji kwa wafugaji
2. Upungufu wa rasilimali watu, fedha na vitendea kazi katika kuendesha shughuli za kila siku.
3. Ukosefu wa masoko ya uhakika.
4. Kukosekana kwa mfumo wa kupanga madaraja ya asali kwa kupima kiwango cha ubora Mkoani.

3.3 Mikakati wa mkoa wa njombe katika ukuzaji wa shughuli za ufugaji nyuki

Mkoa wa Njombe una mkakati wa kukuza shughuli za ufugaji nyuki kama ifuatavyo:-

1. Kuendelea kutoa elimu na hamasa juu ya umuhimu wa shughuli za ufugaji nyuki kiuchumi katika wilaya zote nne za Makete, Njombe, Wanging'ombe na Ludewa.
2. Kuwaunganisha wadau mbalimbali wa shughuli za ufugaji nyuki ili kukuza sekta ya ufugaji nyuki.
3. Kutafuta wahisani/ wawekezaji katika shughuli za ufugaji nyuki.
4. Kuwatambua wafugaji na kuwaunganisha katika vikundi ili wapate elimu na waweze kutafuta masoko na kupanga bei ya mazao ya nyuki.
5. Kutenga fedha kwa ajili ya shughuli za ugani kwa watumishi wa kada mbalimbali mkoani ili kukuza uelewa katika utekelezaji wa shughuli za ufugaji nyuki.
6. Kuandaa mpango wa kuwajengea uwezo watumishi mbalimbali waliopo hadi ngazi ya Kijiji ili waweze kusaidia katika utekelezaji wa shughuli za ufugaji nyuki.
7. Kuandaa vipeperushi vinavyoeleza umuhimu wa matumizi ya mazao ya nyuki na kuvisambaza ili kukuza soko la mazao hayo.

8. Kutoa elimu na kutafuta masoko ya mazao na huduma za nyuki ambazo hazitumiki kwa kiwango cha kutosha mfano huduma za uchavushaji na mazao kama nta, chavua, sumu ya nyuki na gundi ya nyuki.
9. Kutoa elimu kwa wadau mbalimbali wa ufugaji nyuki ili kuweza kupata mahitaji ya bidhaa za ufugaji wa nyuki Mkoani mfano Mafundi seremala kwa ajili ya utengenezaji wa mizinga, mafundi kushona kwa ajili ya ushonaji wa mavazi ya kujikinga na mafundi uashi kwa ajili ya kutengeneza mabomba ya moshi pamoja na patasi za mizinga.
10. Kuwaunganisha wafugaji wa nyuki na taasisi zinazotengeneza vifungashio.
11. Kuhakikisha mazao ya nyuki yanafika sokoni yakiwa na ubora unaotakiwa kwa kuhamasisha uanzishwaji wa wajasiriamali kuanzisha Viwanda vya kufungashia asali.